JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA MTIHANI WA UALIMU CHETI DARAJA LA A (GATCE) 2020

## 614 MAARIFA YA JAMII

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA MTIHANI WA UALIMU DARAJA III A GATCE 2020

# 614 MAARIFA YA JAMII

*Kimechapishwa na:*

Baraza la Mithani la Tanzania,
P.O. Box 2624,
Dar es Salaam, Tanzania.

**© Baraza la Mithani la Tanzania, 2020**

Haki zote zimehifadhiwa.

## YALIYOMO

DIBAJI........................................................................................................ iv

1.0 UTANGULIZI ........................................................................................ 1

2.0 TATHMINI YA MAJIBU YA WATAHINIWA KWA KILA SWALI.......... 2

2.1 SEHEMU A: TAALUMA ........................................................................ 2
2.1.1 Swali Na 1. Stadi Sahili na Tata za Picha na Ramani. ............................... 2
2.1.2 Swali Na 2. Nchi Yetu Tanzania ................................................................ 4
2.1.3 Swali Na 3: Sayari Dunia ............................................................................ 6
2.1.4 Swali Na 4: Nchi Yetu Tanzania ................................................................ 8
2.1.5 Swali Na 5: Sayari Dunia .......................................................................... 10
2.1.6 Swali Na. 6: Mabadiliko ya Kijamii, Kisiasa na Kiuchumi Katika Afrika Huru ....................................................................................................... 13
2.1.7 Swali Na 7: Ukombozi wa Bara la Afrika. .............................................. 16
2.1.8 Swali Na. 8. Utawala na Uchumi wa Kikoloni......................................... 18
2.1.9 Swali Na. 9: Ushirikiano wa Kimataifa .................................................... 20
2.1.10 Swali Na. 10: Vitangulizi vya Ukoloni Tanganyika, Zanzibar Na Kwingineko Afrika. ................................................................................... 22
2.2 SEHEMU B: TAALUMA........................................................................ 24
2.2.1 Swali 11. Nchi Yetu Tanzana .................................................................. 25
2.2.2 Swali 12. Stadi Sahili na Tata za Picha na Ramani .................................. 29
2.2.3 Swali 13. Asili Na Mabadiliko ya Binadamu, Teknolojia Na Mazingira... 32
2.2.4 Swali Na. 14: Utawala na Uchumi wa Kikoloni Afrika. ........................... 35
2.3 SEHEMU C: Ufundishaji ........................................................................ 39
2.3.1 Swali Na. 15: Ufundishaji na Ujifunzaji wa somo. .................................. 39
2.3.2 Swali 16. Maandalizi ya Ufundishaji na Ujifunzaji................................... 42

3.0 UCHAMBUZI WA UFAULU WA WATAHINIWA KWA KILA MADA.. 45

4.0 HITIMISHO ........................................................................................... 46

5.0 MAPENDEKEZO ................................................................................... 46

*Kiambatisho* ............................................................................................... 48

## DIBAJI

Taarifa ya uchambuzi wa majibu ya watahiniwa wa Mtihani wa Maarifa ya Jamii, Ualimu Daraja A, imetayarishwa kwa lengo la kutoa mrejesho kwa walimu tarajali, wakufunzi, watunga sera pamoja na wadau wengine wa elimu. Mitihani ni sehemu mojawapo muhimu ya mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji ambayo huwezesha kutoa tathmini ya namna utekelezaji wa mtaala wa ngazi husika ulivyofanyika. Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika mtihani wa Maarifa ya Jamii utawezesha kutoa mrejesho kuhusu ufundishaji na ujifunzaji wa masomo ya Jiografia na Historia. Majibu ya watahiniwa katika mtihani huweza kuashiria viwango na ubora wa mielekeo, stadi na maarifa ambayo watahiniwa wameweza kuyapata katika kujifunza taaluma na utaalam wa kufundisha katika miaka miwili ambayo wanachuo wamekuwa katika mafunzo.

Katika kufanya uchambuzi wa majibu ya watahiniwa, sababu zilizofanya watahiniwa kujibu maswali vizuri au kushindwa kujibu maswali vizuri zimeainishwa. Uchambuzi wa kila mada na kiwango cha ufaulu katika mada husika pia umefanyika na sababu za mada hizo kufanyika vizuri au vibaya zimebainishwa.

Ni matarajio ya Baraza la Mitihani la Tanzania kuwa, taarifa hii itatoa mrejesho ambao utatumiwa na wadau mbalimbali katika kuboresha mafunzo ya masomo ya Historia na Jiografia katika ngazi ya cheti na pia kushughulikia kasoro zilizobainishwa ili kuboresha ufundishaji na ujifunzaji katika vyuo vya Ualimu na hivyo, kuwezesha kutoa walimu bora wa somo la Maarifa ya Jamii na kuboresha kiwango cha ufaulu kwa walimu tarajali.



Dkt. Charles E. Msonde
**KATIBU MTENDAJI**

## 1.0 UTANGULIZI

Taarifa hii imeandaliwa ili kuwasilisha uchambuzi wa majibu ya watahiniwa wa mtihani wa somo la Maarifa ya Jamii kwa ngazi ya cheti uliofanyika Julai 2020. Maswali ya mtihani yalitungwa kwa kuzingatia Muhtasari wa mwaka 2009 wa somo la Maarifa ya Jamii Ngazi ya Cheti Elimu ya Msingi.

Kwa ujumla kiwango cha ufaulu kwa watahiniwa katika somo la Maarifa ya Jamii kwa mwaka 2020 kilikuwa kizuri kwani asilimia 98.9 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani wa Maarifa ya Jamii walifaulu. Kati ya watahiniwa 3360 waliofanya mtihani, watahiniwa 3326 walifaulu. Hata hivyo watahiniwa 46 (1.4%) walifaulu kwa daraja A na mtahiniwa 1 alipata daraja la F.

Mtihani wa somo la 614 Maarifa ya Jamii uligawanyika katika sehemu A, B, na C. Sehemu A ilikuwa na maswali kumi ambapo maswali matano mada za somo la Jiografia na matano yalitokana na mada za somo la Historia. Mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali yote ambapo kila swali lilikuwa na alama nne. Sehemu B iligawanyika katika maeneo mawili ambayo ni Historia na Jiografia, kila eneo lilikuwa na maswali mawili ambapo mtahiniwa alitakiwa kujibu swali 1 toka kila eneo. Sehemu C (Ufundishaji) ilikuwa na maswali mawili ambapo mtahiniwa alitakiwa kujibu yote. Hivyo mtihani ulikuwa na maswali kumi na sita na mtahiniwa alitakiwa kujibu jumla ya maswali kumi na nne.

Ufaulu wa watahiniwa uligawanywa katika makundi matatu ambayo ni ufaulu mzuri, wastani, na hafifu. Ufaulu mzuri kunaanzia alama 70 hadi 100; kiwango cha wastani alama 40 hadi 69; na kiwango hafifu alama 0 hadi 39.

Katika kufanya uchambuzi na kutafsiri ufaulu wa watahiniwa, aina tatu za rangi zilitumika katika chati, grafu na majedwali ambapo rangi ya kijani inawakilisha ufaulu mzuri, rangi ya njano inawakilisha ufaulu wa wastani na rangi nyekundu inawakilisha ufaulu hafifu.


Taarifa hii inaonesha ufaulu wa watahiniwa kwa kila swali na kila mada. Aidha baadhi ya sampuli za majibu ya watahiniwa waliofanya swali vizuri ama vibaya zimeambatishwa kama vielelezo.

## 2.0 TATHMINI YA MAJIBU YA WATAHINIWA KWA KILA SWALI

### 2.1 SEHEMU A: Taaluma


#### 2.1.1 Swali Na 1. Stadi Sahili na Tata za Picha na Ramani.

Katika swali hili watahiniwa walitakiwa kueleza kwa ufupi sifa nne zinazotofautisha picha na ramani. Uchambuzi wa takwimu za ufaulu zilionesha kuwa watahiniwa wote 3360 walijibu swali hili, na kati ya hao, watahiniwa 1123 (33.4%) walipata alama 0 hadi 1.5. Watahiniwa 1138 (33.9%) walipata alama 2 hadi 2.5, na watahiniwa 1099 (32.7%) walipata alama 3 hadi 4. Kwa ujumla, ufalulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa wa wastani kwa kuwa jumla ya watahiniwa 2237 (66.6%) walipata alama kuanzia 2 hadi 4. Muhtasari wa kiwango cha ufaulu kwa swali hili unaonyeshwa katika Chati Na 1.




**Chati Na. 1 :** *Kiwango cha ufaulu kwa watahiniwa katika Swali la 1.*

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa ulionesha kuwa watahiniwa asilimia 32.7 waliokuwa na ufaulu mzuri walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu sifa za picha na ramani. Aidha, waliweza kuwasilisha majibu yao kwa lugha iliyo wazi. Kwa mfano, baadhi yao walieleza kuwa, picha huchukuliwa kwa kamera lakini ramani huchorwa kwenye karatasi, picha huonesha umbo halisi la kitu lakini ramani huchorwa kuonesha kitu kinavyoonekana, Picha huchukuliwa kwa muda mfupi lakini ramani hutumia muda mrefu kutengeneza. Kielelezo Na. 1.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeweza kujibu vizuri swali la 1.



1. i) Picha ni taswira ya kitu inayochukuliwa kwa kifaa maalumu lakini ramani ni mchoro unaonesha kitu kilivyo kutoka juu.

ii) Picha uchukuliwa kwa kamera lakini ramani uchorwa kwenye karatasi.


iii) Picha uonesha umbo halisi la kitu lakini ramani uchorwa kuonesha kitu kinavyoonekana kutoka juu.

iv) Picha uchukuliwa kwa muda mfupi lakini ramani utumia muda mrefu kuchora.

Kielelezo Na.1.1: Sampuli ya Jibu sahihi katika Swali la 1.

Katika Kielelezo Na. 1.1 mtahiniwa aliweza kueleza kwa usahihi sifa nne zinazotofautisha picha na ramani.

Uchambuzi ulionesha kuwa watahiniwa waliokuwa na ufaulu hafifu walikuwa na maarifa hafifu juu ya mada ambapo walichanganya maelezo kuhusu picha na ramani hasa katika suala la vipimo. Pia watahiniwa wengine walichanganya dhana kati ya ramani na picha za angani. Hata hivyo watahiniwa wengine waliweza kuelezea hoja moja sahihi wengine mbili kati ya nne na zingine hazikukidhi matakwa ya swali. Aidha, baadhi ya hoja za watahiniwa zilikuwa hazijitoshelezi. Kielelezo Na. 1.4 ni sampuli ya jibu lisilo sahihi la mtahiniwa katika swali hili.



| 1 | PICHA | RAMANI |
|---|---|---|
| i | picha ni taswira au kiwakilishi cha kitu. | Ni ufupisho wa eneo kubwa |
| ii | Huchukuliwa katika usawa wa ardhi. | Huchuchuliwa kwa angani. |
| iii | Hazina skeli | Huwa zina skeli kurahisisha usomaji. |
| iv | Hazitumiki katika kujifunza. | Hutumika katika kujifunza. |

Kielelezo Na.1.2: Sampuli ya Jibu la mtahiniwa lisilo sahihi katika Swali la 1.


Kielelezo Na. 1.2, kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kueleza sifa nne zinazotofautisha picha na ramani. Mtahiniwa huyu alichanganya

kati ya picha na ramani na kushindwa kujua faida za picha katika kujifunza na kufundishia.

### 2.1.2 Swali Na 2. Nchi Yetu Tanzania

Swali hili lilitungwa kutoka katika mada ya Nchi yetu Tanzania kipengele cha Tabia ya Nchi. Swali hili lilimtaka mtahiniwa kusoma takwimu za kiwango cha mvua zilizowasilishwa katika jedwali na kisha: (a) kutaja kiasi cha mvua kwa mwaka katika eneo husika, (b) kukokotoa wastani wa kiwango cha mvua kwa mwaka, (c) kueleza aina ya tabia nchi inayowasilishwa na takwimu na kutoa sababu, (d) kueleza kwa kifupi ni nchi gani ya kiafrika takwimu zinaweza kuwa zilichukuliwa.


Jumla ya watahiniwa 3358 (99.9%) walifanya swali hili, kati yao watahiniwa 702 (20%) walipata alama 3 hadi 4. Watahiniwa 934 (27%) walipata alama 2 hadi 2.5 na watahiniwa 1722 (51%) walipata alama 0 hadi 1.5. Takwimu hizi zinaonesha kuwa, kwa ujumla ufaulu katika swali hili ulikuwa wa wastani kwa sababu asilimia 48.7 ya watahiniwa walipata alama zaidi ya 2 kama inavyooneshwa katika Chati Na. 2.




**Chati Na. 2**: *Kiwango cha ufaulu kwa watahiniwa katika Swali la 2.*

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa ulionesha kuwa watahiniwa asilimia 20.9 ya waliofaulu kwa kiwango kizuri walielewa matakwa ya swali na walikuwa na maarifa ya kutosha katika mada hii ya Nchi yetu Tanzania. Watahiniwa waliweza kukokotoa kiwango cha mvua kwa mwaka na kupata


jibu sahihi, walitafuta wastani wa mvua kwa mwaka, walitaja aina ya tabia nchi iliyowakilishwa na takwimu na pia kutaja mfano wa nchi katika bara la Afrika yenye tabia inayofanana na takwimu hizo. Kielelezo Na. 2.1 kinaonesha jibu sahihi katika swali la 2.


2.
2. (a) Mji a
40.8 + 69.0 + 150 + 132 + 205 + 118 + 65 + 69 + 195
226 + 150 + 50.8 = 1585.6 mm
∴ Kiasi cha mvua kwa mwaka mzima ni 1585.6.
(b) Wastani wa kiwango cha mvua (mm) -
Wastani = [illegible]
Wastani = 1585.6 / 12
Wastani = 132.1 mm
(c) Tabia ya nchi inayowakilisha takwimu hizi ni Tabia ya kitropika kutokana na kiwango cha mvua kuwa ni kikubwa katika kipindi cha mwaka mzima
(d) Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo

Kielelezo Na. 2.1: Sampuli ya jibu sahihi katika Swali la 2.

Katika Kielelezo 2.1 mtahiniwa alionesha jinsi alivyokokotoa kiasi cha mvua kwa mwaka mzima pamoja na wastani wa mvua. Aidha, aliweza kutaja aina ya tabia ya nchi inayowakilishawa na takwimu na pia kuweza kutaja nchi ya Afrika yenye hali ya hewa kama hiyo.

Uchambuzi zaidi wa majibu ya watahiniwa ulionesha kuwa asilimia 51.3 ya watahiniwa waliokuwa na ufaulu hafifu hawakuwa na uelewa wa kutosha katika takwimu za hali ya hewa. Baadhi ya watahiniwa walibuni majibu na hivyo kubahatisha kutaja nchi yenye tabia inayowakilishwa na takwimu husika Mfano; kuna waliotaja Malawi, wengine walitoa hoja zisizo sahihi, Mfano: ‘Aina ya tabia nchi ni ya kitropiki kwa sababu halijoto lake limezidi kiwango cha mvua inayotakiwa katika tabia ya nchi hiyo’ hili ni jibu linaloonesha kuwa mtahiniwa hakuwa na maarifa na kupelekea kubuni maelezo. Watahiniwa wengine walijumlisha joto badala ya mvua na hivyo kuandika jibu katika digrii sentigredi (ºC) Kielelezo Na. 2.2 kinaonesha sampuli ya jibu lisilo sahihi kutoka kwa mmoja wa watahiniwa.


7 (a) ~~181.2 (MM)~~ 181.2 mm.

(b) ~~132.133(MM)~~ 132.133 MM.

(c) aina ya tabia nchi ni ya kitropika kwa sababu halijoto lake limezidi kiwango cha mvua inayotoka katika tabia ya nchi hiyo.

(d) Nchi ambayo takwimu hizi zilichukuliwa ni ~~Af Afr Afrika~~ Ethiopia kutokana na kiwango kikubwa kutoka kwenye mstari wa ikweta wenye mvua nyingi.


Kielelezo Na.2.2: Sampuli ya Jibu lisilo sahihi katika Swali la 2.

Katika kielelezo Na 22 mtahiniwa hakuwa na maarifa ya kutosha hivyo badala ya kujumlisha mvua ya kila mwezi mtahiniwa haieleweki alijumlisha namba zipi ambapo alipata jumla ya kiasi cha mvua cha 181.2 mm kwa mwaka ambalo siyo jibu sahihi. Mtahiniwa alitaja *nchi ya Ethiopia kuwa ndiyo takwimu hizi zilichukuliwa na kutokana na kiwango kikubwa kutoka kwenye mstari wa ikweta wenye mvua nyingi*.

### 2.1.3 Swali Na 3: Sayari Dunia


Swali hili lilitoka katika mada ya Sayari Dunia. Swali lilikuwa na vipengele viwili : (a) mtahiniwa alitakiwa kueleza sifa mbili za longitudo, (b) mtahiniwa alitakiwa kufafanua namna mbili ambavyo mistari ya longitudo hutumika.

Uchambuzi wa takwimu za ufaulu ulionesha kuwa watahiniwa 3360 walijibu swali hili, na kati yao watahiniwa 234 (6.96%) walipata alama 0 hadi 1.5. Watahiniwa 584 (17.4%) walipata alama 2 hadi 2.5 na watahiniwa 2542 (75.7) walipata alama 3 hadi 4. Kwa ujumla, ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa mzuri kwa kuwa asilimia 93.1 walipata alama kuanzia 2 hadi 4. Chati Na. 3 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili.




**Chati Na. 3:** *Kiwango cha ufaulu kwa watahiniwa katika Swali la 3*


Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa ulionesha kuwa watahiniwa 2,542 (75.7%) waliokuwa na ufaulu mzuri walikuwa na maarifa ya kutosha na kuweza kutaja sifa mbili za longitudo na namna mbili mistari ya longitudo inavyotumika. Pia watahiniwa walielewa matakwa ya swali na walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusiana na longitudo. Kielelezo Na. 3.1 kinaonesha sampuli ya jibu sahihi kutoka kwa mmoja wa watahiniwa.


3 (a) Kueleza sifa mbili za longitudo.
Longitudo ni mistari ya kubuni inayochorwa kwenye ramani kutoka kaskazini kuelekea kusini.
Sifa za mistari ya longitudo ni;
i/ Hupungua urefu zinapochorwa kutoka ncha nyingine kuelekea ncha nyingine.
3 (a) ii/ Zina sifa ya kukutana zinapochorwa kwenye ramani.
(b) Kufafanua namna mbili ambayo mistari ya longitudo hutumika.
i/ Mistari ya longitudo hutumika kuonyesha mahali katika ramani.
. Mistari ya longitudo inapochorwa kwenye ramani huonesha mahali eneo lilipo.
ii/ Mistari ya longitudo hutumika katika kutafuta muda wa maeneo husika.
- Mistari ya longitudo hutumika katika kutafuta muda au umbali wa maeneo.

Kielelezo Na. 3.1 : Sampuli ya jibu sahihi katika Swali la 3.

Kielelezo Na. 3.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeeleza kwa usahihi sifa mbili za longitudo na matumizi mawili ya longitudo.

Uchambuzi ulionesha kuwa wapo watahiniwa wachache (7.0%) waliokuwa na ufaulu hafifu ambapo walieleza hoja ambazo hazikuwa na usahihi, wapo waliotoa hoja mbili, ama hoja zote nne ambazo zilikuwa na maelezo yasiyo sahihi hivyo kukosa baadhi yake. Aidha, baadhi ya watahiniwa walishindwa kueleza kwa usahihi sifa za longitudo na matumizi ya mistari hiyo. Kielelezo Namba 3.2 ni sampuli ya jibu lisilo sahihi.


3a) i) Ni mstari wa Imajinari
ii) huchorwa toka juu kuenda chini
b) i) hutumika kupata majira ya nchi
ii) hutumika katika kuonesha pande za dunia


Kielelezo Na. 3.2: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika Swali la 3.

Kielelezo Na. 3.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kutaja sifa mbili za longitudo na matumizi mawili kwa usahihi. Inaonekana hakuwa na maarifa ya kutosha katika mada hii kutokana na kuchanganya maelezo kati ya dira na longitudo.

### 2.1.4 Swali Na 4: Nchi Yetu Tanzania


Swali hili lilitoka katika mada ya Nchi Yetu Tanzania. Mtahiniwa alitakiwa kuchanganua kwa kifupi umuhimu wa shughuli nne za kiuchumi zinazofanyika nchini Tanzania.

Jumla ya watahiniwa 3360 walijibu swali hili na ufaulu wao kulikuwa kama ifuatavyo; 46 (1.4%) walipata kati ya alama 0 hadi 1.5, watahiniwa 802 (23.9%) walipata alama kati ya 2 hadi 2.5 na watahiniwa 2512 (74.8%) walipata alama kati ya 3 hadi 4. Uchambuzi ulionesha kuwa ufaulu katika swali hili ukuwa mzuri kwa sababu asilimia 98.7 ya watahiniwa wote walipata alama zaidi ya 2 kama inavyooneshwa katika Chati Na. 4.




**Chati Na. 4:** *Kiwango cha ufaulu kwa watahiniwa katika Swali la 4.*

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa watahiniwa 2572 (74.8%) waliofanya vizuri walikuwa na maarifa ya kutosha katika mada ya Nchi yetu Tanzania, hivyo waliweza kutaja mifano ya shughuli za kiuchumi na kisha kuzielezea umuhimu wake kwa ufasaha. Kielelezo Na. 4.1 kinaonesha sampuli ya jibu sahihi kutoka kwa mmoja wa watahiniwa waliofaulu vizuri swali hili.



04\. Utalii husaidia kutupatia fedha za kigeni na kulitambulisha Taifa letu; katika sekta ya utalii ni moja wapo ya shughuli za kiuchumi ambazo hufanyika nchini Tanzania. hutupatia fedha za kigeni na kulitambulisha Taifa.

Kilimo hutusaidia kupata au kujipatia chakula na pato la Taifa na mtu mmoja mmoja; kama inavyojulikana kuwamba kilimo ni uti wa mgongo katika Taifa letu au katika nchi ya Tanzania ~~kwa~~ hivyo kilimo hutupatia chakula na kipato.


Uchimbaji wa madini husaidia kuinua kipato cha nchi; kutokana na uchimbaji wa madini kutokana na wawekezaji mbalimbali ambao wamewekeza katika uchimbaji wa madini hutoa ajira kwa wananchi na huongeza pato la nchi.

Uvuvi hutusaidia au husaidia watu kujipatia vitoweo; watu huweza kujipatia vitoweo pamoja na fedha za kujikimu au kuendesha maisha yao au maisha yetu.

Kielelezo Na.4.1: Sampuli ya jibu sahihi la mtahiniwa katika Swali la 4.

Kielelezo Na. 4.1 kinaonesha majibu ya mmoja wa watahiniwa aliyejibu vizuri swali kwa kutaja shughuli za kiuchumi na kisha kuelezea umuhimu wake.

Hata hivyo, wapo watahiniwa 46 (1.4%) waliokuwa na ufaulu hafifu ambapo watahiniwa wengi kati ya hawa waliandika majibu yasiyokamilika ipasavyo. Takwimu zilionesha kuwa wapo walioelezea bila kutaja shughuli husika ya uchumi. Wengine walitaja shughuli za uchumi na hawakuelezea umuhimu wa shughuli hizi. Mfano mtahiniwa alitaja *Utalii, kilimo, viwanda* na *Biashara.* Uchambuzi zaidi wa majibu ya watahiniwa ulionesha kuwa wengine waliandika hoja zisizo sahihi kama Kielelezo Na. 4.2 kinavyoonesha.


4. i/ Kuongeza pato la taifa, ambalo husaidia Tanzania kupanua ujenzi wa miundo mbinu
ii/ Kulipa wafanyakazi wote wa serikali. Hii kuhamasisha utendaji kuwa mzuri.
iii/ Zinainua uwezo wa maisha ya kila mtu ili uweze kuwa na maisha mazuri lazima ufanye kazi
iv/ Kutoa ajira kwa watu wote. Husaidia katika kujikimu kimaisha

Kielelezo Na.4.2: Sampuli ya jibu la mtahiniwa lisilo sahihi katika Swali la 4.


Kielelezo Na. 4.2 kinaonesha sampuli ya majibu la mtahiniwa ambaye hakuzingatia matakwa ya swali kwa kutoa maelezo ya jumla bila kutaja kwanza shughuli ya kiuchumi ambayo ingemwezesha kuelezea umuhimu wake ili kuwe na muunganiko wa maelezo na shughuli hiyo.

### 2.1.5 Swali Na 5: Sayari Dunia

Swali hili lilitungwa kutoka katika mada ya Sayari Dunia. Swali hili liliwataka watahiniwa kubainisha majanga manne ya asili na kisha kueleza kwa kifupi namna ambavyo athari zake zinaweza kupunguzwa.


Watahiniwa 3360 (100%) walijibu swali hili, kati yao watahiniwa 128 (3.8%) walipata alama 0 hadi 1.5, watahiniwa 557 (16.6%) walipata alama 2 hadi 2.5 na watahiniwa 2675 (79.6%) walipata alama kati ya 3 hadi 4. Uchambuzi wa takwimu ulionesha kuwa watahiniwa asilimia 96.2 walikuwa

na ufaulu mzuri kuanzia alama 2 hadi 4 kama inavyooneshwa katika Chati Na. 5




**Chati Na. 5:** *Kiwango cha ufaulu katika Swali Na. 5.*

Uchambuzi wa majibu wa watahiniwa ulionesha kuwa watahiniwa 2675 (79.6%) waliofanya vizuri waliweza kubainisha majanga manne ya asili na kisha kueleza kwa kifupi namna ambavyo athari zake zinaweza kupunguzwa. Kielelezo Na. 5.1 kinaonesha mfano wa majibu sahihi kutoka kwa mmoja wa watahiniwa.


5 i. mafuriko
Ni hali ya maji kuacha njia yake ya kawaida na kuenea katika maeneo mbalimbali
njia ya kupunguza athari
Kujenga makazi kwa mpangilio ili kutengeneza njia rasmi za maji kupita.


iii. Tetemeko la ardhi
Ni hali ya mtikisiko wa ardhi juu ya uso wa dunia na ndani ya uso wa dunia unaosababisha ardhi kupasuka au kutitia
Njia
Kujenga majengo mafupi ili kuepusha vifo kutokana na tetemeko la ardhi.

iv. Milipuko ya kivolkano
Ni hali ya kuongezeka kwa kiwango cha joto ndani ya uso wa ardhi kunakotokana na kani mvutano na kusababisha kuyayusha kwa miamba na kutengeneza ujiuji unaoitwa magma unatoka nje huwa lava
njia
Kuepuka kujenga makazi karibu na milima

Kielelezo Na. 5.1: Sampuli ya jibu sahihi kwa Swali la 5

Katika kielelezo Na. 5.1, mtahiniwa alizingatia matakwa ya swali kwa kutoa mifano ya majanga ya asili na kisha kuelezea jinis ambavyo athari zake zinaweza kupunguzwa.

Uchambuzi zaidi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa wapo watahiniwa wachache (3.8%) ambao walikuwa na ufaulu hafifu. Watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kutosha katika mada ya Sayari Dunia. Baadhi walitoa majibu yasiyokidhi matakwa ya swali. Wengine walishindwa kuandika lugha fasaha katika hoja zao. Aidha, wapo ambao walishindwa kukamilisha hoja nne na kuishia hoja mbili, wengine hoja tatu nazo zikiwa na mapungufu. Kielelezo Na. 5.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa yasiyo sahihi kwa swali la 5.



5 (i) Jangwa
Tunaweza kupunguza janga hili kwa kutokukata miti ayo.
(ii) Kupotea kwa viumbe
Ili janga hili lisitokee ambalo linaweza kuwa kama chanzo cha ufanisi ni vyema wanaindi wasichome miitu ayo.
(iii) Ukame
Kuzuia kukata miti ayo.
(iv)


Kielelezo Na.5.2: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika Swali la 5.

Kielelezo Na 5.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa ambaye hakuwa na maarifa ya kutosha. Mtahiniwa aliandika majibu yasiyoendana na mahitaji ya swali, aidha uandishi wa maneno katika hoja zake haukuwa sahihi.

### 2.1.6 Swali Na. 6: Mabadiliko ya Kijamii, Kisiasa na Kiuchumi Katika Afrika Huru


Swali la 6 lilitoka katika mada ya Mabadiliko ya Kijamii, Kisiasa na Kiuchumi Katika Afrika Huru. Watahiniwa walitakiwa kuelezea kwa kifupi mabadiliko manne yanayoonesha mafanikio katika nchi za kiafrika baada ya kujipatia uhuru kutoka kwa wakoloni.

Watahiniwa 3360 (100%) walijibu swali hili, kati yao watahiniwa 105 (3.1%) walipata alama 0 hadi 1.5, watahiniwa 350 (10.4%) walipata alama 2 hadi 2.5 na watahiniwa 2905 (86.5%) walipata alama kati ya 3 hadi 4. Uchambuzi wa takwimu unaonesha kuwa watahiniwa asilimia 96.9 walikuwa na ufaulu mzuri wa kuanzia alama 2 hadi 4 kama inavyooneshwa katika Chati Na. 6.




**Chati Na. 6:** *Ufaulu wa watahniwa katika swali la 6.*

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa ulionesha kuwa watahiniwa asilimia 96.9 waliofaulu kwa kiwango kizuri walikuwa na maarifa ya kutosha katika mada ya Mabadiliko ya Kijamii, Kisiasa na Kiuchumi Katika Afrika Huru. Hivyo waliweza kutaja mabadiliko katika makundi manne na kuelezea kwa ufasaha mafanikio yake katika nchi na wengine walielezea mafanikio kisha wakatoa mifano ya miundombinu. Kielelezo Na. 6.1 kinaonesha mafanikio katika nchi za kiafrika baada ya kujipatia uhuru kutoka kwa wakoloni.



6 i/ Mabadiliko ya elimu, Waafrika waliboresha elimu tofauti na ubaguzi uliokuwepo wa wakoloni. Hivyo kila mtu alipata elimu baada ya uhuru.

ii/ Mabadiliko kwenye muundo mbinu. Waafrika baada ya uhuru waliboresha muundo mbinu kama barabara, reli, viwanja vya ndege pia na bandari.


iii/ Mabadiliko kwenye Viwanda. Wakoloni walijenga viwanda kwa ajili ya kupunguza uzito wa malighafi kusafirisha kwenda ulaya. Lakini baada ya uhuru Waafrika waliboresha viwanda kwa kuzalisha bidhaa.

iv/ Mabadiliko kwenye kilimo. Baada ya uhuru Waafrika walifanya kilimo kama ni kitega uchumi ambacho kitawaletea maendeleo

Kielelezo Na.6.1: Sampuli ya jibu sahihi kwa swali la 6.

Kielelezo Na. 6.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeweza kuelezea mafanikio katika nchi za kiafrika baada ya kujipatia uhuru kutoka kwa wakoloni.

Hata hivyo watahiniwa 105 (3.1%) waliokuwa na ufaulku hafifu hawakuwa na maarifa ya kutosha katika mada hii. Uchambuzi zaidi wa majibu ya watahiniwa ulionesha kuwa baadhi yao walitoa maelezo yasiyoendana na swali husika. Aidha, baadhi walielezea hali ya waafrika kipindi cha ukoloni na wengine walitoa hoja zisizo sahihi. Mfano wa majibu ya mtahiniwa kuhusu mabadiliko manne yanayoonesha mafanikio katika nchi za kiafrika baada ya kujipatia uhuru kutoka kwa wakoloni yalikuwa: *Kutaifishwa kwa elimu, elimu ya shule ya msingi ilifanywa kuwa miaka saba badala ya nane, elimu ya Sekondari ilifanywa kuwa elimu ya kujitegemea, wakuu wa shule za msingi na sekondari walikuwa ni wananchi*. Kielelezo Na. 6.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa ambaye hakujibu swali la 6 kwa usahihi.



6. (i) Waafrika walipata elimu na ujuzi mbalimbali katika shughuli mbalimbali.
(ii) Baadhi ya tamaduni za kiafrika zilipotea kabisa.
(iii) Waafrika walianza kujitegemea na kujiongoza wenyewe
(iv) Waafrika walijifunza mbinu mbalimbali za kupambana na hali ya maisha


Kielelezo Na. 6.2: Sampuli ya jibu lisilo sahihi kwa swali la 6.

Katika Kielelezo Na. 6.2 mtahiniwa alitoa maelezo yasiyo sahihi na hivyo kushindwa kuelezea mabadiliko manne yanayoonesha mafanikio katika nchi za kiafrika baada ya kujipatia uhuru kutoka kwa wakoloni.

### 2.1.7 Swali Na 7: Ukombozi wa Bara la Afrika.


Swali hili lilitoka katika mada ya Ukombozi wa Bara la Afrika. Swali liliwataka watahiniwa kueleza kwa kifupi mbinu nne zilizotumiwa na nchi mbalimbali za kiafrika katika harakati za ukombozi wa Bara la Afrika.

Uchambuzi wa takwimu za kufaulu ulionesha kuwa watahiniwa 3360 (100%) walijibu swali hili. Kiwango cha ufaulu kilikuwa kama ifuatavyo; watahiniwa 1899 (56.5%) walipata alama kuanzia 3 hadi 4, watahiniwa 759 (22.6%) walipata kuanzia alama 2 hadi 2.5 na watahiniwa 702 (20.9%) walipata alama kuanzia 0 hadi 1.5. Uchambuzi zaidi ulionesha kuwa ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa mzuri kwa sababu asilimia 79.1 ya watahiniwa wote walipata alama zaidi ya 2 kama inavyooneshwa katika Chati Na. 7.





**Chati Na. 7:** *Kiwango cha ufaulu kwa swali la 7*

Uchambuzi wa majibu ya watahiwa unaonesha kuwa, watahiniwa (56.5%) walikuwa na ufaulu mzuri kwa kuwa walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu ukombozi wa Bara la Afrika, hivyo waliweza kuelezea mbinu nne zilizotumiwa na nchi mbalimbali za kiafrika katika harakati za ukombozi wa Bara la Afrika. Pia walielewa matakwa ya swali na kutumia maarifa waliyonayo kuwasilisha majibu sahihi kwa kutaja mbinu hizo na kisha kuzielezea. Kielelezo Na. 7.1 kinaonesha majibu sahihi ya mmoja wa watahiniwa katika swali hili.


7. i) majadiliano;- mfano Tanganyika, mwalimu Julius nyerere alitumia mbinu hii katika kudai harakati za ukombozi kwa kushirikiana na watanganyika wengine.
ii) mbinu ya kivita;- mataifa mengi yalipigana na kumwaga damu ambapo walipigana vita mfano Kenya.
iii) mbinu ya mapinduzi;- mfano zanzibar walim pindua sultani na kuweza kumshinda katika wakati wala wanyama 1963.
iv) mbinu ya majadiliano na kivita;- mataifa mbalimbali ya afrika yalitumia mbinu hizi katika harakati za kudai uhuru.

Kielelzo Na. 7.1: Sampuli ya jibu sahihi kwa swali la 7.

Hata hivyo uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kwamba baadhi ya watahiniwa (20.9%) waliokuwa na ufaulu hafifu hawakuwa na maarifa ya kutosha katika mada hii na wengine walishindwa kuelewa matakwa ya swali. Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa watahiniwa waliandika majibu ya kubuni ambapo mengine hayakuwa sahihi na hayakuwa na maelelezo kabisa. Mfano wa majibu kuhusu Mbinu nne zilizotumiwa na nchi mbalimbali za kiafrika katika harakakati za ukombozi wa Bara la Afrika walitaja ; *Upinzani, Mkutano wa Berlin, Vita na Uvamizi.* Kielelezo Na. 8.2 kinaonesha majibu ya mmoja wa watahiniwa yasiyo sahihi kwa swali la 8.



7. i) Kuheshimu mila na destuni za Kiafrika
ii) Kukomesha biashara ya utumwa.
iii) Kusaini mikataba
iv) Usaliti

Kielelezo Na.7.2: Sampuli ya majibu yasiyo sahihi kwa swali la 7.

Katika kielelezo Na. 7.2 mtahiniwa alitoa hoja zisizoendana na matakwa ya swali.


### 2.1.8 Swali Na. 8. Utawala na Uchumi wa Kikoloni.

Swali hili lilitoka katika mada ya Utawala na Uchumi wa kikoloni. Katika swali hili watahiniwa walitakiwa kufafanua kwa kifupi sababu nne zilizowafanya waingereza kupendelea zaidi mfumo wa utawala wa mlango wa nyuma katika makoloni yao. Watahiniwa wote 3360 (100%) walifanya swali hili; kati yao watahiniwa 1382 (41.1%) walipata alama 3 hadi 4. Aidha takwimu zilionesha kuwa watahiniwa 600 (17.9%) walipata alama 2 hadi 2.5 na watahiniwa 1378 (41%) walipata alama 0 hadi 1.5. Kwa ujumla watahiniwa katika swali hili walikuwa na ufaulu wa wastani kwa sababu asilimia 59 ya watahiniwa walipata alama zaidi ya 2 kama inavyooneshwa kwenye Chati Na. 8.




**Chati Na. 8:** *Kiwango cha ufaulu katika swali la 8.*


Watahiniwa 1382(41.1%) waliokuwa na ufaulu mzuri katika swali hili walieleza kwa ufasaha sababu za waingereza kupendelea zaidi mfumo wa utawala wa mlango wa nyuma. Watahiniwa hawa walionesha kuwa na maarifa ya kutosha kuhusu ukoloni. Aidha uchambuzi unaonesha kuwa watahiniwa walitambua matakwa ya swali hivyo, waliwasilisha hoja kwa usahihi. Kielelezo Na. 8.1 kinaonesha majibu sahihi ya mmoja wa watahiniwa katika swali la 8.


8. Zababu za mfumo wa utawala wa mlango wa nyuma.
i/ Upungufu wa watumishi; waingereza hawakuwa na watumishi wengi watakao kuendeleza na kusimamia mambo yao.
ii/ Kuepuka migomo na migogoro, kati yao na Waafrika. Walitumia machifu ili kuepuka migogoro katika yao na waafrika, ili waafrika waendelee kuwaamini machifu wao.
iii/ Tatizo la lugha, au mawasiliano, hii ni kwasababu waingereza hawakuwa wanajua lugha ya kiswahili hivyo walitumia machifu [illegible]
iv/ Kuepuka gharama za kusimamia, na hivyo ilikuwa rahisi kwani hawakutumia gharama kubwa, zaidi ya kutoa mshahara kidogo kwa machifu.

Kielelezo Na.8.1: Sampuli ya jibu sahihi katika swali Na. 8.

Kielelezo Na. 8.1, kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeeleza kwa usahihi sababu nne zilizowafanya waingereza kupendelea zaidi mfumo wa utawala wa mlango wa nyuma katika makoloni yao.

Hata hivyo, watahiniwa 1378 (41.0%) ambao walikuwa na ufaulu hafifu walieleza hoja zisizoendana na matakwa ya swali. Uchambuzi zaidi wa majibu ya watahiniwa ulionesha kuwa kiwango hiki hafifu kilisababishwa na watahiniwa kutokuwa na maarifa ya kutosha kuhusu dhana husika. Aidha baadhi yao walitoa hoja chache kinyume na matakwa ya swali. Mfano wa majibu ya mtahiniwa aliyetoa hoja tatu alielezea kuwa waingereza walipendelea zaidi mfumo wa utawala wa mlango wa nyuma katika makoloni yao kwa kuwa; *'hawakutaka kuonesha uvamizi wowote katika makoloni yao', kuchunguza jinsi wenzao wanavyoishi'* na *'kutaka kufanya uvamizi'* Vilevile wapo waliotoa hoja nne zisizo sahihi, wengine walitoa hoja tatu ama mbili na kati ya hizo nyingine zilikuwa na makosa.



8 i) Kutowapo wa afrika nafasi ya kutawala
Walitumia mfumo huo ili Kuendelea ku
wanyonya waafrika kiuchumi.

ii) Kuendelea kupata wafanyakazi katika masha
mba yao.
Walitumia utawala huo ili kuweka kodi
ambazo zingewafanya waafrika kuendelea kuwatu
mikia.
iii) Kupata nafasi ya kuendelea kuchunguza
mali zilizopo nchini.
Walitumia utawala huu ili kupata maml
aka ya kuchunguza mali walizonazo watanza
nia.

iv) ili kuwanyonya kiuchumi


Kielelezo Na. 8.2: Sampuli ya jibu lisilo sahihi kwa swali la 8.

Kielelezo Na. 8.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kukidhi matakwa ya swali.

### 2.1.9 Swali Na. 9: Ushirikiano wa Kimataifa


Swali hili lilitoka katika mada ya Ushirikiano wa Kimataifa na lililenga kupima ufahamu wa wanafunzi kaktika ushirikiano wa kimataifa. Mtahiniwa alitakiwa kueleza kwa kifupi sababu nne za kuundwa kwa Umoja wa Afrika.

Jumla ya watahiniwa 3360 (100%) walijibu swali hili na kati yao, watahiniwa 692 (20.6%) walipata alama 3 hadi 4. Watahiniwa 2439 (72.6%) walipata alama 2 hadi 2.5 na watahiniwa 229 (6.8%) walipata alama 0 hadi1.5. Uchambuzi wa takwimu za watahiniwa unaonesha ufaulu mzuri katika swali hili kwani asilimia 93.2 walipata alama kuanzia 2 hadi 4 kama inavyooneshwa katika Chati Na. 9.




**Chati Na. 9:** *Kiwango cha ufaulu katika swali la 9.*

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa ulionesha kuwa 692 (20.6%) walifanya vizuri kwa kuwa walielewa swali na hivyo kujibu kulingana na mahitaji ya swali. Aidha, tathmini mbalimbali Mfano, majaribio ya mara kwa mara, mitihani ya ndani pamoja na maandalizi mazuri ya mtihani wa taifa, vinaweza kuwa vimeongeza umahiri wa kujibu maswali kwa watahiniwa. Kielelezo Na. 9.1 Kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa miongoni mwa waliojibu kwa usahihi swali la 9.


9. Sababu za kuundwa umoja wa Afrika
i) Kudumisha ulinzi, usalama na ushirikiano miongoni mwa nchi wanachama

ii) Kutatua migogoro
Kuundwa kwa umoja wa Afrika lengo lake pia ni kutatua migogoro iliyokuwa ikiendelea, hasa ya kisiasa
Mfano: Somalia, Burundi, Sudani na Kongo


iii) Kupiga vita umaskini
lengo kuundwa kwa umoja wa mataifa ili kuwa ni kubuni sera zitakazoinua nchi kutokana na nchi nyingi Afrika ni maskini.

iv) Kuinua uchumi na ushirikiano
Katika kuendeleza hali ya kipato miongoni mwa Mataifa mbalimbali katika Bara la Afrika, lengo ilikua ni kuinua uchumi wa nchi wanachama.

Kielelezo Na. 9.1: Sampuli ya jibu sahihi la swali la 9.

Kielelezo Na. 9.1 kinaonesha ya mtahiniwa aliyeeleza kwa usahihi sababu nne za kuundwa kwa Umoja wa Afrika.

Hata hivyo, watahiniwa 229 (6.8%) ambao walikuwa ufaulu hafifu, baadhi yao hawakuelewa matakwa ya swali. Uchambuzi zaidi wa majibu ya watahiniwa ulionesha kuwa watahiniwa hawakuwa na maarifa ya kutosha kwani wengine walishindwa kuelezea kwa ufasaha sababu za kuundwa kwa Umoja wa Afrika au kutoa hoja chache kuliko matakwa ya swali. Aidha uchambuzi wa kina unaonesha kuwa wapo ambao hawakujibu kabisa swali hili, hivyo kupata alama 0. Kielelezo Na. 9.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyekuwa na hafifu ufaulu.


9 i kuondoa matabaka
ii kuwa na soko huria
iii kuonesha mshikamano baina yao
iv kila mtu kuwa huru kuenda nchi nyingine

Kilelezo Na. 9.2: Sampuli ya jibu lisilo sahihi kwa swali la 9.


Kielelezo Na. 9.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyetoa maelezo bila kuandika hoja kwanza. Mfano; mtahiniwa alitakiwa kutaja hoja zifuatazo kisha kuzielezea; *Kudumisha amani, kutokomeza ujinga, umasikini na maradhi miongongi mwa nchi wanachama, kuondoa ainza zote za ubaguzi, na kuimarisha misingi ya demokrasia barani Afrika* na *kuweza kuungana na kuwa na serikali moja ya nchi za Afrika.*

### 2.1.10 Swali Na. 10: Vitangulizi vya Ukoloni Tanganyika, Zanzibar Na Kwingineko Afrika.

Swali la 10 lilitungwa kutoka katika mada ya Vitangulizi vya Ukoloni Tanganyika, Zanzibar na Kwingineko Afrika. Swali hili lilimtaka mtahiniwa kutoa hoja nne kwa nini mataifa ya Ulaya yalivamia na kuligawa bara la Afrika.


Jumla ya watahiniwa 3359 (99.9%) walijibu swali hili vizuri na viwango vya ufaulu katika swali hili ni kama ifuatavyo: Watahiniwa 701 (20.9%) walipata alama 0 hadi 1.5, watahiniwa 980 (29.2%) walipata alama 2 hadi 2.5 na watahiniwa 1678 (50%) walipata alama 3 hadi 4. Takwimu hizi

zilionesha kuwa ufaulu katika swali hili ulikuwa mzuri kwa sababu asilimia 79.2 ya watahiniwa walipata alama kuanzia 2 hadi 4 kama inavyooneshwa katika Chati Na. 10.




**Chati Na. 10:** *Kiwango cha ufaulu katika swali la 10.*

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa watahiniwa (79.1%) waliofanya vizuri walikuwa na maarifa ya kutosha katika mada ya Vitangulizi vya Ukoloni Tanganyika, Zanzibar na Kwingineko Afrika, hivyo waliweza kutaja sababu za mataifa ya Ulaya kuvamia na kuligawa Bara la Afrika. Kielelezo Na. 10.1 kinaonesha sampuli ya jibu sahihi kutoka kwa mmoja wa watahiniwa waliofanya vizuri swali hili.



10. i) Kutafuta malighafi
Baada ya vita kuu ya pili ya Dunia mataifa mengi yaliathirika kiuchumi hivyo kuona njia bora ni kuja barani Afrika kwa ajili ya kupata malighafi za viwanda huko Barani Ulaya


ii) Kutafuta masoko ya bidhaa zao
Kutokana na bidhaa kuzalisha kwa wingi baada ya mapinduzi ya viwanda walihitaji kupata sehemu kwa ajili ya kuuza bidhaa zao.
Mfano: Nguo, vyombo

iii) Kutafuta vibarua wa bei nafuu
Walihitaji wafanyakazi kwa ajili ya viwanda vyao huko Ulaya hivyo waliwakamata vijana wenye nguvu na kwenda nao.

iv) Kutafuta maeneo kwa ajili ya uwekezaji
Pia wakoloni walihitaji maeneo yenye rutuba kwa ajili ya kulima mazao ya Biashara kwa ajili ya kupata malighafi na kusafirisha kupeleka Ulaya.

Kielelezo Na.10.1. Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 10.

Watahiniwa 701 (20.9%) walikuwa ufaulu hafifu. Ufaulu huu ulisababishwa na watahiniwa kutokuwa na maarifa ya kutosha katika mada hii. Kwa mfano, mtahiniwa alitaja sababu za kugawa bara la Afrika kuwa ni; ‘K*utawala bara la Afrika’, ‘Kueneza tamaduni zao’, ‘Kuepuka migogoro baina ya wakoloni’ na ‘uwepo wa mto nile.’* Aidha, uwezo mdogo wa kuwasilisha majibu kulingana na matakwa ya swali na wengine kutotimiza idadi ya majibu iliyotakiwa. Kielelezo Na. 10.2 ni sampuli ya majibu yasiyo sahihi kwa swali la 10.


10 Sababu za kuligawa bara la Afrika
i) Kuepusha migogoro miongoni mwao
ii) kufuta kwa biashara ya utumwa
iii) kuondoa biashara ya utumwa
iv)

Kielelezo Na. 10.2: Sampuli ya majibu yasiyo sahihi kwa swali la 10.

Kielelezo Na. 10.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa ambaye alishindwa kuzingatia matakwa ya swali. Mtahiniwa hakutaja hoja Mfano kutafuta masoko ya bidhaa zao, kutafuta wafanyakazi watakaowalipa ujira mdogo, kutafuta maeneo ya madini na kuzielezea bali alizitaja tu.


## 2.2 SEHEMU B: Taaluma

Sehemu hii ilikuwa na maswali manne yaliyogawanywa katika vipengele viwili; kipengele cha Jiografia ambacho kilikuwa na maswali mawili na kipengele cha Historia maswali mawili. Mtahiniwa alitakiwa kuchagua swali moja katika kila kipengele. Kila swali katika sehemu B lilikuwa na jumla ya alama 15. Ufaulu wa watahiniwa katika sehemu hii uligawanywa katika makundi matatu kulingana na alama walizopata watahiniwa. Watahiniwa waliopata alama 0 hadi 5.5 walikuwa na ufaulu hafifu katika swali husika. Aidha, watahiniwa waliopata alama 6 hadi 10 walikuwa na ufaulu wa wastani, na watahiniwa waliopata alama 10.5 hadi 15 walikuwa na ufaulu mzuri.

### 2.2.1 Swali 11. Nchi Yetu Tanzana

Swali la 11 lilitoka katika mada ya Nchi Yetu Tanzania. Katika swali hili watahiniwa walitakiwa kupendekeza njia tano endelevu zinazoweza kutumika kutunza mazingira.

Jumla ya watahiniwa 1089 (32.4%) walijibu swali hili na viwango vyao vya ufaulu vilikuwa kama ifuatavyo: Watahiniwa 11 (1.0%) walipata alama 0 hadi 5.5, watahiniwa 363 (33.3%) walipata alama 6 hadi 10 na watahiniwa 715 (65.7%) walipata alama 10.5 hadi 15. Uchambuzi wa takwimu za ufaulu ulionesha kuwa watahiniwa katika swali hii walikuwa na ufaulu mzuri kwa sababu asilimia 98.9 ya watahiniwa waliofanya swali hili walifaulu swali hili kama inavyooneshwa katika Chati Na. 11.




**Chati Na. 11:** *Kiwango cha ufaulu katika swali la 11.*


Uchambuzi wa majibu ulionesha kuwa watahiniwa (65.7%) walikuwa na ufaulu mzuri katika swali hili. Uchambuzi zaidi ulionesha kuwa ufaulu huu mzuri ulisababishwa na watahiniwa kuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada ya Nchi yetu Tanzania. Aidha, uwezo wa watahiniwa kujieleza, pamoja na uwezo wa kujibu maswali ya insha vilisababisha kiwango hiki cha ufaulu. Kielelezo Na. 11.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mmoja wa watahiniwa aliyefanya vizuri.

11 Mazingira. Hivi ni vitu vyote ambavyo vinazunguka maisha ya mtu vyaweza kuwa miti, mimea, mawe, maji, viumbe hai. Vitu hivi vyote ni sehemu ya mazingira hivyo ni bora kuvilinda kwa vizazi vya badaE yafuatayo ni mapendekezo juu ya njia za kuhifadhi mazingira.

Kupanda miti kila unapokata miti hiki ni kitendo cha kuweka miti katika ardhi baada ya kukata miti mwingine hii itasaidia kupata mvua katika maeneo kwa wakati; Hivyo tunapopanda miti tunasaidia kutunza mazingira yetu.

Kufuga mifugo michache katika eneo ni kitendo cha kuwa na mifugo ambayo ni tasholezi katika eneo husika na sio kuwa na mifugo mingi na huku eneo ni dogo huweza kuleta mmomonyoko wa ardhi. Hivyo watu tufuge mifugo michache ili kulinda ardhi zetu na mazingira kwa ujumula

Viwanda kujengwa sehemu ambazo sio za makazi ya watu, hivyo basi ni kitendo cha uanzishaji wa viwanda nje ya mji ili kuepusha maji na sumu zinazotolewa na viwanda kuwa fikia watu katika makazi. Hii husaidia kupunguza uharibifu wa mazingira.



Kujenga kwa kufuata njia au.
Mwongozo wa mipango miji ni kitendo cha
kuwa na ujenzi sehemu inayohusiwa kujengwa
na sio kulundikana kuweza kuleta shida ya
kimazingira. Hivyo watu wajenge kwa mpangilio.
Kulima kilimo cha matuta ili kuepusha
mmomonyoko wa udongo ni kilimo ambacho
hutumia kuinua baadhi ya ardhi hivyo
kuzuia mmomonyoko wa udongo kutokea
mfano sehemu yenye mteremko ni vizuri
kulima kwa kutengeneza matuta ili kupunguza
mmomonyoko huo.
Hivyo basi mazingira tunahitaji
tuyatunze ili na sisi yatutunze kwa maana
sisi maisha yetu yana tegemea kwa kiasi
kikubwa uwepo wa mazingira mfano
watu wakikata miti ovyo mvua zitakua
za kuhangaika hivyo shughuli kama
kilimo kukwama.

Kielelezo Na. 11.1: Sampuli ya jibu sahihi la mtahiniwa kwa swali la 11.

Uchambuzi pia ulionesha kuwa pamoja na watahiniwa wengi kuwa na ufaulu mizuri, wapo watahiniwa (1.0%) waliopata alama hafifu. Kiwango hiki kilionesha kuwa watahiniwa walikosea baadhi ya hoja miongoni mwa zile walizoelezea. Kwa mfano mtahiniwa alitaja njia endelevu zinazoweza kutumika kutunza mazingira kuwa ni ; *'kutofuga ng'ombe wengi katika eneo dogo' 'Uchomaji wa taka', 'Kufukia mashimo', 'kutotupa taka au kuchafua katika vyanzo vya maji' na 'kufyeka vichaka'* Kielelezo Na. 11.2 kinaonesha majibu yasiyo sahihi ya mmoja wa watahiniwa.

11. Mazingira ni jumla ya mambo yote yanayoizunguk jamii. Kwenye mazingira huwa na upatikanaji wa mambo mbalimbali au vitu. Njia endelevu zinazoweza kutumika kutunza mazingira ni

Upandaji wa miti. Ili kutunza mazingira ni lazima kupandwe miti ya kutosha. Miti hii husaidia hii nchi kupata mvua za kutosha na kuepuka janga la ukame. Pia miti husaidia kuleta hewa safi na mazingira ya kuvutia katika jamii.

Kata miti otesha miti. Hii ni njia endelevu ya utunzaji wa mazingira kwani mtu anapokata miti na kuotesha miti husaidia kuepukana na majanga tofauti tofauti ambayo yangetokea kama asingeotesha miti mingine.

Njia nzuri ya ukusanyaji wa taka: Njia njia husaidia jamii kukusanya taka katika mazingira yao na kuzichoma, au kuzitumia kwa matumizi mengine yaani (Recycline) Hivyo hufanya iwe njia endelevu katika kutunza mazingira.

Kufuata njia za kitaalamu katika kilimo na viwand Pia wakulima na wamiliki wa viwanda wafuate njia za kitaalamu ili kuto haribu mazingira kwa namna yoyote. Mfano ufugaji holela, upandaji wa mazao kwa kutumia mbolea zenye kemikali. Hivyo wakifuata njia za kitaalamu watafuata watatufadhi mazingira vizuri

Kutoa Elimu kwa jamii: Serikali inatakiwa kutoa elimu ya utunzaji endelevu wa mazingira. Wanajamii wakishaelimika na kupata faida za utunzaji wa mazingira, basi lengo hili la mazingi safi na salama linawezekana.

Hivyo basi mazingira ni kitu muhimu sana kwa maisha ya kila siku utunzaji wake ni walazim


Kielelezo Na. 11.2: Sampuli ya majibu kwa swali la 11.

Katika Kielelezo Na. 11.2 mtahiniwa alitaja hoja baadhi zikiwa na kujirudia na nyingine zikikosa maelezo ya kujitosheleza.

### 2.2.2 Swali 12. Stadi Sahili na Tata za Picha na Ramani

Swali la 12 lilitoka katika mada ya Stadi Sahili na Tata za Picha na Ramani. Swali hili lililenga kupima nyanja ya ufahamu ambapo mtahiniwa alitakiwa kueleza vipengele muhimu vinavyowezesha ramani kutumika kwa ufanisi.

Jumla ya watahiniwa 2,274 (99.7%) walijibu swali hili na viwango vyao vya ufaulu vilikuwa kama ifuatavyo: Watahiniwa 6 (0.3%) walipata alama 0 hadi 5.5, watahiniwa 633 (27.8%) walipata alama 6 hadi 10 na watahiniwa 1635 (71.9%) walipata alama 10.5 hadi 15. Uchambuzi wa takwimu za ufaulu ulionesha kuwa ufaulu katika swali hili ulikuwa mzuri kwa sababu asilimia 99.7 ya watahiniwa waliofanya swali hili walifaulu. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili la 11 kinaoneshwa katika Chati Na. 12.




**Chati Na. 12 :** *Kiwango cha ufaulu katika swali la 12.*

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa watahiniwa 1635 (71.9%) waliofaulu swali hili walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada ya Stadi Sahili na Tata za Picha na Ramani. Aidha, uwezo mkubwa wa watahiniwa kujieleza pamoja na kujibu maswali ya insha vilisababisha kiwango hiki cha ufaulu. Uchambuzi zaidi wa majibu ya watahiniwa ulionesha kuwa watahiniwa waliweza kutaja na kuelezea vipengele muhimu na kuchora vielelezo vyake kwa usahihi. Kielelezo Na. 12.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mmoja wa watahiniwa.


12. Ramani, ni mchoro unaochorwa katika uso wa kitu mfano karatasi, ardhini, ukutani na kwenye kitambaa kuonesha sura ya nchi. Kuna aina kuu mbili za ramani ambazo ni ramani za takwimu na ramani za kitopografia ambazo huonesha maumbile mbalimbali ya nchi. Vipengele muhimu vya ramani vifuatavyo:-

Skeli, ni kipimio cha ramani ambacho huonesha uwiano kati ya umbali halisi katika ardhi na umbali katika ramani. Skeli huwasilishwa katika njia tatu ambazo ni njia ya sentensi au maneno mfano sentimeta moja katika ramani kuwakilisha kilomita 3 kwenye ardhi, pia njia ya uwiano mfano 1:250,000, na njia ya tatu ni ile ya mstari kuonesha umbali.

Dira, ni uelekeo wa Dunia katika pande zake kuu nne ambazo ni Kaskazini, Kusini, Magharibi na Mashariki. Pia Dunia imegawanywa katika pande nyingine nyingi ndogondogo. Katika ramani dira huonesha ramani imeelekea upande upi ambapo huonesha kaskazini. Kama mfano wetu unavyofafanua.




Ufunguo, ni kipengele muhimu katika ramani ambacho hufafanua shughuli, na mambo yaliyooneshwa kwenye ramani hivyo kumfanya yule anayesoma ramani kutambua ujumbe uliopo na kuweza kubaini shughuli zilizopo katika ramani hiyo mfano; kilimo, ufugaji, madini, uvuvi, viwanda na biashara mfano:




Kichwa cha ramani, hiki ni kipengele ambacho hukaa juu kabisa ya ramani ili kutambulisha kile kilichopo kwenye ramani iliyochorwa mfano: RAMANI YA TANZANIA KUONESHA MILIMA NA MABONDE. Hivyo kichwa cha ramani hufafanua dhumuni la ramani.


Flemu, ni uzio unaozungushiwa kwenye ramani kwa umbo la mstatili au mraba kulingana na mchoro wa ramani uliochorwa. Katika ramani ni muhimu kuizungushia flemu ili kuipa ramani mwonekano mzuri na hivyo kuvutia na kuonesha vipengele vyema.

Hivyo basi, ni lazima kwa mchoraji wa ramani kuweka vitu hivyo katika ramani ili iweze kueleweka na kurahisisha usomaji wake. Hivyo kufikisha ujumbe uliokusudiwa kwa watu.

Kielelezo Na. 12.1: Sampuli ya jibu sahihi kwa swali la 12.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa ulionesha kuwa watahiniwa 6 (0.3%) waliopata alama hafifu, walikosa maarifa ya kutosha katika mada hii. Hivyo walishindwa kuwasilisha majibu yanayojitosheleza na kusababisha kupata

alama hafifu katika hoja zao. Uchambuzi zaidi wa majibu ya watahiniwa ulionesha kuwa wengine waliandika idadi ya hoja zilizohitajika katika swali na kukosea aidha hoja mbili ama hoja tatu kati ya hizo kutokana na kutokuwa sahihi. Mfano wa hoja za mtahiniwa ambazo hakupata alama ni '*Matumizi sahihi ya mistari ya Longitudo' na 'matumizi sahihi ya mistari ya Latitudo'* Kielelezo Na. 12.2 kinaonesha sampuli ya majibu yasiyo sahihi kwa swali la 12.


12. Ramani ni vitu au ni muundo wa kitu pia
ambao unaonesha nchi au Sehemu mbalimbali za
maeneo husika. Vifuatavyo ni vipengele muhimu
u vinavyowezesha ramani kutumika ufanisi
ni kama zifuatazo.
Fremu; ili ramani iweze kutumika kwa
ufanisi lazima pawepo na fulemu ndipo ramani
itaweza kutumika. huyo fulemu ni kipengele
kimoja wapo cha ramani
Pande kuu za dunia, kipengele kingine
kinacho patikana kwenye ramani ni pande
kuu nne za ramani ~~amaz~~ ambazo ni Mashariki
Magharibu Kaskazini na Kusini hizi ndo huone
sha ufanisi wa ramani.
Ufunguo; hii pia ni kipengele moja wapo cha
ramani ambacho uwezo kuonesha ramani kutumika
kwa ufanisi. Ufunguo lazima kuwepo kama kipe
ngele ili kukuonesha vitu vinavyopatikana ndani
ya ramani.
Mistari ya Contua, kipengele kingine amb-
ambacho upatikana kwenye ramani ambayo mist
ari hii uonesha pale au kwenye ramani ili
kuweza kujua urefu ambayo vimo kwenye ramani
. Hivyo basi hivi ni mojawapo ya vipengele muhimu
vinavyo wezesha ramani kutumika kwa ufanisi.


Kielelezo Na. 12.2: Sampuli ya majibu yasiyoridhisha kwa swali la 12.

Katika Kielelezo Na. 12.2 mtahiniwa aliwasilisha hoja zilizojirudia na nyingine zilikosa maelezo ya kujitosheleza. Aidha majibu yaliyoandikwa hayakuwekewa michoro yoyote ya kuonyesha mifano ya vipengele muhimu vinavyowezesha ramani kutumika kwa ufanisi.

### 2.2.3 Swali 13. Asili Na Mabadiliko ya Binadamu, Teknolojia Na Mazingira.

Swali la 13 lilitoka katika mada ya Asili na Mabadiliko ya Binadamu, Teknolojia Na Mazingira. Swali hili lililenga kupima nyanja ya ufahamu ambapo mtahiniwa alitakiwa kueleza mabadiliko matano yaliyotokea katika maisha ya binadamu wakati wa zama za chuma.

Jumla ya watahiniwa 2259 (67.2%) walijibu swali hili kwa usahihi kwa sababu walielewa matakwa ya swali. Viwango vya ufaulu katika swali hili ni kama ifuatavyo: watahiniwa 94 (4.2%) walipata alama 0 hadi 1.5, watahiniwa 1385 (61.3%) walipata alama 6 hadi 10 na watahiniwa 780 (34.5%) walipata alama 10.5 hadi 15. Kwa ujumla ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa mzuri kwani asilimia 95.8 ya watahiniwa walikuwa na ufaulu wa wastani au zaidi. Chati Na. 13 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali la 13.




**Chati Na. 13:** *Kiwango cha ufaulu katika swali la 13.*

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa ulionesha kuwa watahiniwa waliofaulu swali hili kwa kiwango kizuri walikuwa na maarifa ya kutosha katika mada ya Asili na Mabadiliko ya Binadamu, Teknolojia na Mazingira. Aidha, watahiniwa walielewa matakwa ya swali, pia uwezo wa kujieleza

pamoja na kujibu maswali ya insha vilisababisha kiwango hiki cha ufaulu. Uchambuzi zaidi wa majibu ya watahiniwa ulionesha kuwa watahiniwa waliweza kuelezea mabadiliko yaliyotokea katika maisha ya binadamu wakati wa zama za chuma. Kielelezo Na. 13.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mmoja wa watahiniwa.

13. Zana za chuma alianzisha makazi ya kudumu
na jamii kama za wapare walijihusisha na
shughuli za uhunzi ambapo walijulikana
kwa jamii zingine na kupata faida
kutokana na kubadilishana bidhaa hizo
na jamii zingine zisizokuwa na ujuzi
Kukua na kuongezeka kwa uzalishaji
Mali; kutokana na matumizi bora ya zana
za chuma watu walijishughulisha na kilimo
Walipata chakula kingi na kingine cha ziada
Walitumia kubadilishana na jamii zingine
ambazo hazijihusishi na kilimo. Mfano jamii
za wamasai zinazojulikana katika utendaji
wa shughuli za kiufugaji
Kuanzishwa kwa shughuli za kibiashara.
Jamii ambazo zilijulikana kuwa ni maarufu
katika utengenezaji wa zana za chuma
zilibadilishana bidhaa hizo kama visu, majembe
mashoka, panga na jamii ambazo zilikuwa
hazijihusishi na shughuli za uhunzi kama
jamii za pwani ambazo zilijihusisha sana
na kilimo cha mazao kama karafuu, nazi
na kahawa.
Kuimarika kwa shughuli za ulinzi na -
Usalama katika jamii; katika jamii ambazo
zilijihusisha na uhunzi wa uchongaji wa
Vifaa mbalimbali kama mikuki, mishale, visu
zilisababisha kupata silaha za kujilinda na
kupelekea kuimarika kwa ulinzi na
Usalama wa wanajamii na mali zao.
Kwahiyo; kuna mabadiliko mengi katika
Maisha ya binadamu wakati wa zama za chuma
Ambayo yanaendelea mpaka katika maisha ya

Kielelezo Na.13.1: Sampuli ya jibu sahihi la swali 13.

Aidha, wapo watahiniwa wachache (4.2%) waliokuwa na ufaulu hafifu, kimetokana na kutokuwa na maarifa ya kutosha katika mada hii. Uchambuzi pia unaonesha kuwa miongoni mwa watahiniwa hawakuelewa matakwa ya swali, hivyo kuandika majibu yasiyohusiana na matakwa ya swali. Kielelezo Na. 13.2 kinaonesha majibu yasiyo sahihi ya mmoja wa watahiniwa.

13 Mabadiliko ya binadamu - hizi ni hatua ambazo binadamu wakwanza alipitia kama inavyoelezwa na mwanasayansi Dakta Charles dawn binadamu wakwanza alikuwa sokwe akawa anabadilika hadi. Sasa. Hatua hizo ni mabadiliko aliyopitia.

Pliothepikasi. hii ni hatua ya kwanza kabisa ya mabadiliko ambayo binadamu wa kwanza aliatumia akitembea kwa miguu na mikono yaani [illegible] anaishi katika misitu minene akikwea juu ya miti kutafuta matunda.

Ramathepikasi - Ni hatua ya pili ya mabadiliko ya binadamu ambayo binadamu huyu alianza kusimama kwa miguu miwili kuangalia maadui zake lakini bado alitembea kwa miguu minne

Zinjathropasi ni hatua ya tatu ya mabadiliko ya binadamu ambayo binadamu alikuwa amepita hatua hii aliweza ~~kutembea kwa~~ kusimama kwa miguu miwili na mwili wake ulikuwa bado una manyoya mengi ubongo wa kichwa ulikuwa unaanza kupungua.

Australothepikasi robustusi - hii ni hatua ya nne ambayo binadamu alipitia alianza kutembea kwa miguu miwili mwili wake ulianza kupunguza manyoya aliendelea kukua na kubadilika taratibu.

Homo habilisi - Ni hatua ya tano aliyopitia binadamu wakale. hatua hii mwili wa binadamu ulizidi kubadilika zaidi na kutoka kwenye usokwe hadi kufikia hali ya ubinadamu ikiwani kubatilika kwa mkia na kichwa kupungua.

Kwa ujumla mabadiliko ya binadamu yanatimia katika hatua kumsaba ikiwa ni pamoja na homo erektasi na homo sapien. Ambapo ndiye binadamu wa sasa hivi na hii ndio inahitimisha mabadiliko hayo


Kielelezo Na. 13.2: Sampuli ya jibu lisilo sahihi kwa swali la 13.

Kielelezo Na. 13.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyetaja hoja zisizokuwa sahihi akielezea hatua za mabadiliko ya mwanadamu kwa jumla hivyo kutoka nje ya matakwa ya swali lililotaka mabadiliko katika zama za chuma.

### 2.2.4 Swali Na. 14: Utawala na Uchumi wa Kikoloni Afrika.

Swali la 14 lilitoka katika mada ya Utawala na Uchumi wa Kikoloni Afrika, na likiwataka watahiniwa kueleza mbinu tano ambazo wakoloni walizitumia katika kuimarisha utawala wao barani Afrika.


Jumla ya watahiniwa 1,099 (32.7%) walifanya swali hili. Viwango vya ufaulu katika swali hili vilikuwa kama ifuatavyo, watahiniwa 616 (56.1%) walipata alama 0 hadi 1.5, watahiniwa 413 (37.6%) walipata alama 6 hadi 10 na watahiniwa 70 (6.3%) walipata alama 10.5 hadi 15. Kwa ujumla ufaulu katika swali hili ni wa wastani kwani watahiniwa asilimia 43.9 walipata alama 2 hadi alama 4. Ufaulu wa watahiniwa umeoneshwa katika Chati Na. 14.




**Chati Na. 14:** *Viwango vya ufaulu katika swali la 14.*

Uchambuzi ulionesha kuwa, watahiniwa 616 (56.1%) waliopata kiwango hafifu cha ufaulu walikuwa hawana maarifa ya kutosha katika mada hii. Baadhi ya watahiniwa walichanganya kati ya utawala wa kikoloni na uchumi wa kikoloni hivyo kutoa maelezo ya uchumi wa kikoloni.

Watahiniwa wengine hawakuelewa matakwa ya swali, hivyo kuandika majibu yasiyo sahihi. Hoja nyingine pia zilijirudia katika aya za majibu ya watahiniwa. Mfano kuna walioandika, *‘mbinu ya kijeshi’* na *‘mbinu ya kuanzisha ngome za kijeshi’* katika aya tofauti. Kielelezo Na. 14.1 kinaonesha majibu yasiyo sahihi ya mmoja wa watahiniwa.



14. Wakoloni ni watu waliokuja Afrika kwa lengo la kututawala kwa mabavu. Kama vile wajerumani, waingereza, wafaransa na wareno. Zifuatazo ni mbinu ambazo wakoloni walizitumia katika kuimarisha utawala wao barani Afrika.

Kunyang'anywa ardhi yenye rutuba. Hii ni mbinu waliyoitumia wakoloni katika kuimarisha utawala wao, wakoloni waliwanyang'anya waafrika ardhi yao na kuanza kuitumia wenyewe na waafrika kuwa wafanyakazi katika ardhi yao wenyewe.

Kuwatipisha kodi. Hii pia ni mbinu nyingine waliyoitumia wakoloni katika kuimarisha utawala wao, wakoloni walianza kuwadai kodi wa afrika ingawa ni ardhi yao na ni makazi yao kama vile kodi ya kichwa.

Kuwatumikisha waafrika katika mashamba yao. Waafrika walikuwa wanafanya kazi katika mashamba ya wakoloni kwa kutumikishwa sana hivyo walishindwa kufanya kazi zao zingine.

Kuwalipa ujira mdogo. Wakoloni waliwaajiri waafrika katika maeneo yao hivyo kuweza kuwalipa ujira mdogo sana ambao haukuweza kukidhi mahitaji yao hata kidogo.

Kuwatumia waafrika kama chombo cha usafirishaji. Waafrika walisafirisha bidhaa mbalimbali kwenye maeneo yenye masafa marefu.

Hivyo basi, Wakoloni waliwatumikisha sana waafrika ambao hawakuwa na hatia ipokuwa walivamia eneo la waafrika.

Kielelezo Na. 14.1: Sampuli ya majibu yasiyojitosheleza kwa swali la 14.

Kielelezo Na. 14.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyepata alama hafifu kutokana na kuchanganya wazo la Utawala wa kikoloni na Uchumi wa kikoloni.

Hata hivyo watahiniwa asilimia (6.4%) waliofaulu swali hili kwa kiwango kizuri waliweza kutaja na kuelezea mbinu tano ambazo wakoloni walitumia katika kuimarisha utawala wao barani Afrika

Aidha uwezo wa kujieleza na kujibu maswali ya insha kwa kufuata hatua sahihi vimesababisha kupata kiwango hiki cha ufaulu . Kielelezo Na. 14.2 kinaonesha sampuli ya majibu sahihi ya mtahiniwa aliyefanya vizuri.

14 Ukoloni ni hali ya nchi yenye nguvu kutawala ~~ny~~ nchi nyingine katika nyanja ya kiuchumi, kisiasa, kiutamaduni na kibiashara pamoja na kimawasiliano pia. Wakoloni ni watu kutoka Ulaya kuja barani Afrika kwa ajili ya kuimarisha shughuli zao. Zifuatazo ni mbinu zilizotumiwa na wakoloni kuimarisha utawala wao.

Mbinu ya kijeshi, ni aina ya mbinu iliyotumiwa na wakoloni katika maeneo ambayo yalikuwa na upinzani mkubwa dhidi ya utawala wao, mfano wa maeneo hayo yalikuwa Kilimanjaro, Tabora, Iringa na Tanga.

Mbinu ya kusaini mikataba ya ulaghai, walitumia mbinu hii kwa sababu viongozi wa jadi wa kiafrika hawakuwa wanajua kusoma na kuandika. Hivyo ikawafanya wakoloni kuwasainisha viongozi hao ili kufanikisha maslahi yao pasipo viongozi hao kujua mfano wa mkataba uliosainiwa ni wa Karl Peters na Chief Mangungo wa Msovero mwaka 1884 ~~na~~ mkataba mwingine ni wa Harry Johnstone na Mandara wa Kilimanjaro.

Mbinu ya kuchagua watawala kwa niaba ya wananchi, walitumia mbinu hii ili kupata viongozi watakaosaidia kufanikisha shughuli zao, mfano walichagua maliwali, majumbe na maliwali.

Mbinu ya kujenga ngome za kijeshi, walitumia mbinu hii pia katika maeneo yaliyoonesha upinzani dhidi ya utawala wao, mfano ngome hizi walizijenga mipakani na sehemu za Tabora maeneo ya Choyo.

Mbinu ya kuanzisha vyombo vya ukandamizaji kama vile mahakama, sheria, magereza na jeshi. Lengo kuu la kuanzisha vyombo hivi ilikuwa ni kufanikisha maslahi yao.

Hivyo basi utawala wa kikoloni haukuwa na manufaa yeyote kwa Waafrika kwa sababu ulikuwa utawala wa kinyonyaji, ubaguzi, ukandamizaji, hivyo ukapelekea Waafrika kupoteza tamaduni zao pamoja na rasilimali zao.

Kielelezo Na. 14.2: Sampuli ya jibu sahihi la swali la 14.


## 2.3 SEHEMU C: Ufundishaji

Sehemu hii ilikuwa na maswali mawili ya ufundishaji kutoka katika masomo ya Jiografia na Historia. Mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali yote katika sehemu hii, ambapo kila swali lilikuwa na alama 15. Ufaulu wa watahiniwa katika sehemu hii uligawanywa katika makundi matatu kulingana na alama walizopata. Watahiniwa waliopata kuanzia alama 0 hadi 5.5 walikuwa na ufaulu hafifu katika swali husika. Aidha, watahiniwa waliopata alama kati ya 6 hadi 10 walikuwa na ufaulu wa wastani, na iwapo watahiniwa walipata alama kati ya 10.5 hadi 15 walikuwa na ufaulu mzuri.

### 2.3.1 Swali Na. 15: Ufundishaji na Ujifunzaji wa somo.

Swali la 15 lilitoka katika mada ya Ufundishaji na Ujifunzaji wa somo. Swali hili lilimtaka mtahiniwa kutoa hoja tano kutathmini udhaifu wa matumizi ya njia ya mhadhara kama mbinu ya kufundishia somo la Jiografia.

Jumla ya watahiniwa 3359 (99.9%) kati ya 3360 walifanya swali hili na viwango vya ufaulu vilikuwa kama ifuatavyo: Watahiniwa 87 (2.6%) walipata alama 0 hadi 1.5, watahiniwa 648 (19.3%) walipata alama 6 hadi 10 na watahiniwa 2941 (78.1%) walipata alama 10.5 hadi 15. Kwa ujumla ufaulu katika swali hili ulikuwa mzuri kwa sababu asilimia 97.4 walifaulu vizuri kwa kupata alama kuanzia 6 hadi 15. Chati Na. 15 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali la 15.




**Chati Na. 15:** *Kiwango cha ufaulu katiika swali la 15.*

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa ulionesha kuwa (78.1%) waliokuwa na kiwango kizuri cha ufaulu walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada ya ufundishaji. Aidha watahiniwa walikuwa na uwezo wa kujieleza pamoja mpangilio mzuri wa kujibu maswali ya insha. Uchambuzi zaidi wa majibu unaonesha kuwa watahiniwa waliokuwa na ufaulu mzuri walielewa matakwa ya swali na waliweza kujibu vizuri.


15. Mhadhara ni mbinu mojawapo anayotumia mwalimu wakati wa kufundisha kwa kufundisha watu wengi kwa wakati mmoja. Hii ni njia ya ufundishaji iliyo shirikishi kwa wanafunzi. Yafuatayo ni madhaifu ya kutumia njia ya mhadhara kama mbinu ya kufundishia somo la jiografia :-

Haimshirikishi mwanafunzi. Mbinu hii ya - mhadhara haimshirikishi mwanafunzi kwa kuwa mwanafunzi ni msikilizaji tu na kupokea yale - yanayosemwa na mwalimu. Hivyo mbinu hii haimushirikishi mwanafunzi katika tendo ujifunzaji.

Hutumia muda mrefu. Mwalimu anapofundisha mbinu hii ya mhadhara huweza kuchukua muda mwingi kumalizika na kuwafanya wanafunzi kulichukia somo kwa sababu hawapati fursa ya kujifunza kwa vitendo.

Pia mbinu hii huwachosha wanafunzi. Wanafunzi huchoka kwa urahisi katika tendo la ufundishaji na ujifunzaji somo la jiografia kwa sababu hawawashughulishi katika mchakato mzima wa ujifunzaj hii hutokana na kwamba mwalimu yeye ndiyo kisima cha maarifa.

Vilevile mbinu hii haiwajengei wanafunzi - udadisi na uwezo wa kufikiri juu ya kile wanachofundishwa na mwalimu. Hii hutokana na kwamba hawajishughulishi katika tendo la ufundishaji na ujifunzaji somo la jiografia bali huwa kama wasikilizaji tu kwa kumsikiliza mwalimu anachofundisha kwa sababu wanafunzi hajifunzi kwa vitendo.




Pia mbinu hii ya mhadhara haimjengei -
mwanafunzi kumbukumbu ya kudumu juu ya
kile anachofundishwa na mwalimu. Hii ni kwa -
sababu mwanafunzi hatumii milango yake ya
fahamu katika tendo la ufundishaji na ujifunzaji
kwa mfano kungusa, kuoja, kunusa pia hata -
kuhisi. Matumizi ya milango ya fahamu kwa
mwanafunzi huweza kumjengea kumbukumbu ya
kudumu juu ya kile ~~ana~~ alichofundishwa.
Kwahiyo katika mchakato wa ufundishaji na
ujifunzaji somo la jiografia matumizi ya njia
ya mhadhara kama mbinu ya kufundishia huwa
na madhaifu mengi. Hivyo yuwapasa walimu
kutumia njia zingine za kufundishia ambazo ni
shirikishi, yaani zinawashirikisha wanafunzi
katika tendo ufundishaji somo la jiografia kwa
mfano mbinu ya maswali na majibu, majadiliano,
ziara, kazi mradi pamoja mbinu ya jaribio ili
kuwafanya wanafunzi wajifunze kwa vitendo.

Kielelezo Na.15.1: Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 15.

Kielelezo Na. 15.1 kinaonesha majibu sahihi ya mtahiniwa alielezea kwa ufasaha udhaifu wa matumizi ya njia ya mhadhara kama mbinu ya kufundishia.

Kwa upande mwingine watahiniwa 87 ambao ni sawa na asilimia 2.6 waliokuwa na ufaulu hafifu walikuwa hawana maarifa ya kutosha ya njia ya mhadhara katika ufundishaji. Uchambuzi pia ulionesha kuwa miongoni mwa watahiniwa hao hawakuelewa matakwa ya swali, hivyo waliandika baadhi ya majibu yasiyo sahihi na kukosa baadhi ya hoja Uchambuzi wa kina unaonesha kuwa baadhi ya watahiniwa walitoa mapendekezo ya namna ya kuboresha mbinu ya mhadhara badala ya kutoa udhaifu wa njia hiyo. Mfano *'kutumia lugha nyepesi na inayoeleweka', 'kutumia sauti kubwa', 'kutumia maelezo ya moja kwa moja', 'kuhakikisha usikivu darasani' na 'mwalimu kuhusianisha mada na mazingira ya wanafunzi'.* Kielelezo Na. 15.2 kinaonesha baadhi ya majibu yasiyo sahihi kwa swali namba 15.



15. Mhadhara, Ni mbinu ya ufundishaji ambayo huitumia mwalimu katika utendaji wake wa kazi. Yafuatayo ni madhaifu ya mbinu ya mhadhara kama njia ya kufundishia somo la Jiografia;-

Kutokujenga dhana iliyokusudiwa kwa wanafunzi: Njia ya mhadhara huwa kama ya masimulizi ambayo mwalimu huwa ni mtendaji mkuu na huzungumza bila kuhojiwa hivyo ni ngumu kutambua kama wanafunzi wamejenga dhana iliyokusudiwa.

Hamushirikishi mwanafunzi katika utendaji wa shughuli ya kujifunza. Mbinu hii si rafiki na haishauriwi sana kutumika wakati wa kufundisha kwani mwalimu huwa msemaji mkuu na mwanafunzi ni msikilizaji tu.

Hailengi kumjengea ubunifu na udadisi mwanafunzi; Masimulizi yasiyo na ushirikisho kwa mjifunzaji hushindwa kukuza fikra juu ya kile alichojifunza.

Hutumia muda mwingi katika uwasilishaji wake; Muda mwingi hutumika katika kuhakisha maudhui yanamfikia mlengwa.

Kutokufikiwa kwa malengo mahususi yaliyokusudiwa; Masimulizi yasiyohitaji mchango wa maswali humchosha mwanafunzi na kujikuta kasinzia na hivyo mwalimu kushindwa kulifikia lengo lililotarajiwa.

Hatahivyo; kujenga udadisi, stadi, ubunifu na ujuzi kwa mwanafunzi ni vema kutumia mbinu shirikishi ili kumpa nafasi ya kuhoji na kudadisi mambo mbalimbali juu ya kile anachojifunza na hii itasaidia kufikiwa kwa malengo mahususi yaliyopangwa na mtaala.


Kielelezo Na. 15.2 Sampuli ya majibu yasiyo sahihi kwa swali la 15.

Kielelezo 15.2 kinaonesha kuwa mtahiniwa aliweza kuelezea baadhi ya udhaifu wa matumizi ya njia ya mhadhara kama mbinu ya kufudishia somo la jiografia. Mtahiniwa pia alishindwa baadhi ya hoja hivyo kukosa nyingine na kupelekea kupata alama hafifu.

### 2.3.2 Swali 16. Maandalizi ya Ufundishaji na Ujifunzaji.


Swali la 16 lilitoka katika mada ya Maandalizi ya ufundishaji na ujifunzaji. Swali hili liliwataka watahiniwa kuainisha njia tano zinazoweza kutumika kujipatia zana za kufundishia na kujifunzia somo la Historia.


Jumla ya watahiniwa 3,358 (99.9%) walijibu swali hili. Ufaulu katika swali hili ni kama ifuatavyo: watahiniwa 76 (2.3%) walipata alama 0 hadi 5.5, watahiniwa 1,227 (36.5%) walipata alama 6 hadi 10 na watahiniwa 2,055 (61.2%) walipata alama 10.5 hadi 15. Kwa ujumla ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa mzuri kwani asilimia 97.7 ya watahiniwa walikuwa waliopata alama 6.0 hadi alama 15 kama inavyooneshwa katika Chati Na. 16.




**Chati Na. 16:** *Kiwango cha ufaulu katika swali la 16.*

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa ulionesha kuwa ufaulu mzuri ulitokana na watahiniwa kuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada ya Maandalizi ya ufundishaji na ujifunzaji. Aidha watahiniwa walionekana kuwa na uwezo wa kujieleza pamoja na uzoefu wa kujibu maswali ya insha vitu ambavyo vimesababisha kuwa na ufaulu mzuri. Kielelezo Na. 16.1 kinaonesha sampuli ya majibu sahihi ya mtahiniwa.



16. Zana, Ni jumla ya vifaa anavyotumia mwalimu wakati wa ufundishaji na ujifunzaji ili kurahisisha kueleweka kwa somo kwa urahisi mfano ramani, chati, mawe, redio, vitabu na majarida mbalimbali. Zifuatazo ni njia za upatikanaji wa zana za kufundishia na kujifunzia somo la Historia.


Huweza kupatikana kwa njia ya kufa
ragua mfano Ramani, Vitabu, Michoro,
hivyo Mwalimu huweza kutumia mazingira
yanayomzunguka kupata zana za kufu
ndishia historia kwa kutumia makumbusho
yaliyo hali ya eneo hilo ambayo yanaen
dana na mada husika.
Huweza kupata zana kwa njia ya
kununua kwenye maduka au kwa watu
binafsi wenye zana hizo mfano luninga,
Redio, Michoro, huweza kununuliwa na
mwalimu kupata zana za kufundishia
Somo la Historia.
pia huweza kupatikana kwa njia ya
kukusanya katika mazingira mfano Mawe,
vijiti, mimea, hivyo Mwalimu na Wanafunzi
huweza kushirikiana katika kufanikisha
zoezi hili la kukusanya zana.
Kupatikana kwa njia ya kutengeneza
mfano Kuchonga, Kuchora, Kusuka, hivyo
basi Mwalimu huweza kukusanya makunzi
ya zana husika na kutengeneza kwa kufuata
vipimo maalumu mfano huweza kutenge
neza zana ya kinyago, na kufanikisha
kufikisha malengo mahususi.
Kupata zana kwa njia ya kuazima na
kukodisha, zana kama vile Projekta, Luninga
Vinasa sauti, huweza kupatikana kwa kuazi
ma au kukodisha kwa wamiliki wa vitu hivyo
yaweza kuwa Shule jirani au kwenye Jamii.
Hitimisho, katika ufundishaji na ujifu
nzaji wa Somo la historia ni muhimu kuweza
na matumizi ya zana, kwakuwa zana hizo

Kielelezo Na. 16.1: Sampuli ya majibu sahihi kwa swali la 16.

Kielelezo Na. 16.1 kinaonesha majibu sahihi ya mtahiniwa alielezea kwa ufasaha njia tano zinazoweza kutumika kujipatia zana za kufundishia na kujifunzia somo la Historia.

Hata hivyo wapo watahiniwa wachache (2.3%) waliokuwa na ufaulu hafifu walionesha kutokuwa na maarifa ya kutosha katika mada hii. Miongoni mwa watahiniwa walitaja hoja zisizo sahihi mfano 'kutembelea Maktaba' na wengine hoja zilikuwa sahihi isipokuwa maelezo hayakukidhi matakwa ya swali ;. Aidha, uchambuzi zaidi unaonesha kuwa majibu ya baadhi ya hoja za watahiniwa hazikuwa sahihi, hivyo walikosea hoja hizo. Kielelezo Na. 16.2 kinaonesha majibu yasiyo sahihi kwa swali hili.


16. (i) Kuazima mf. ~~jobo~~ jopo la wataalamu.
(ii) Kununua mf. vinyago
(iii) ~~Kufaragua~~ Kuchora mfano ramani
(iv) Kuchonga mf. sokwe

Kielelezo Na. 16.2: Sampuli ya majibu yasiyojitosheleza kwa swali la 16.

Kielelezo hiki kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyepata alama hafifu kutokana na kuandika majibu yasiyojitosheleza kwa swali la 16. Mtahiniwa alitaja tu hoja nne badala ya kuelezea kwa mfumo wa insha.

## 3.0 UCHAMBUZI WA UFAULU WA WATAHINIWA KWA KILA MADA

Uchambuzi wa viwango vya ufaulu wa watahiniwa katika mada zote ulionesha kuwa, ufaulu wa watahiniwa ulikuwa mzuri katika mada kumi. Mada hizo ni: Maandalizi ya ufundishaji na ujifunzaji (97.7%), Ufundishaji na ujifunzaji wa somo (97.4%), Mabadiliko ya kijamii, Kisiasa na Kiuchumi katika Afrika Huru (96.8%), Asili na Mabadiliko ya Binadamu, Teknolojia na Mazingira (95.8), Sayari Dunia (94.6%), Ushirikiano wa Kimataifa (93.1%), Stadi Sahili na Tata za Ramani (83.1%), Nchi Yetu Tanzania (82.1%), Vitangulizi vya Ukoloni Tanganyika, Zanzibar Na Kwingineko Afrika (79.1%), Ukombozi wa Bara la Afrika (79.1%) na mada ya Utawala na Uchumi wa Kikoloni Afrika ambayo ufaulu wake ulikuwa (51.4%) Rejea Kiambatisho.

Kwa ujumla, watahiniwa waliweza kufaulu katika mada kadhaa kutokana na sababu mbalimbali. Kati ya sababu za kufaulu ni umahiri wa kutosha wa watahiniwa katika mada hizo. Aidha uwezo wa kutambua matakwa ya maswali mbalimbali na kuandika inavyopasa. Ufaulu huu mzuri unadhihirisha kuwa, wakufunzi walikamilisha mada zao na kuwapa

watahiniwa maarifa na weledi wa kutosha na hivyo, kuwaandaa vema kwa ajili ya mtihani wa Taifa wa Maarifa ya Jamii.

## 4.0 HITIMISHO

Kwa ujumla, mtihani wa Ualimu Daraja A katika somo la Maarifa ya Jamii mwaka 2020 ulizingatia muhtasari wa masomo ya Jiografia na Historia wa mwaka 2009. Maswali yote yalizingatia ngazi zote za majazi ya utambuzi zikiwemo; nyanja ya maarifa, ufahamu, matumizi, uchambuzi, tathmini na uundaji. Ufaulu wa watahini katika mtihani huo ulikuwa mzuri na wa kuridhisha katika mada 10. Aidha, ufaulu katika mada moja ulikiwa wa wastani na hapakuwa na mada ambayo ufaulu wake ulikuwa hafifu.

Uchambuzi huu ulibainisha changamoto mbalimbali ambazo hazina budi kutafutiwa ufumbuzi kwa lengo la kurekebisha mapungufu yaliyojitokeza na hivyo, kuboresha mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji wa masomo ya Historia na Jiografia. Changamoto hizo ni pamoja na watahiniwa wachache kutoelewa maswali hivyo kushindwa kutoa majibu sahihi kulingana na matakwa ya maswali. Pia, baadhi ya watahiniwa kukosa umakini na hivyo kuchanganya hoja ambazo hazihusiani kabisa na maswali husika. Aidha, baadhi ya watahiniwa hawakuwa na maarifa ya kutosha katika baadhi ya maswali jambo lililowafanya washindwe kujibu baadhi ya maswali kwa ufanisi.

Taarifa hii ya uchambuzi itasaidia kutoa mrejesho kuhusu namna mada za somo la Maarifa ya Jamii zilivyofundishwa vyuoni na hivyo, kuonesha maeneo yenye upungufu katika ufundishaji na ujifunzaji ili kutoa fursa nzuri zaidi kwa wakufunzi, wanachuo na wakuza mitaala kuboresha mitaala, ufundishaji na ujifunzaji kwa mada ambazo watahiniwa hawakufanya vizuri ili kuboresha ufaulu wa watahiniwa kwa miaka ijayo.

## 5.0 MAPENDEKEZO

Ili kuboresha zaidi kiwango cha ufaulu katika mtihani wa Maarifa ya Jamii inapendekezwa kuwa:

(a) Wakufunzi wawasisitize watahiniwa kuhusu umuhimu wa kusoma kwa makini maswali kabla ya kuyajibu. Hii itasaidia watahiniwa kutoa majibu yanayoendana na mahitaji ya maswali waliyoulizwa na hivyo kuepuka kuchanganya dhana wakati wa kujibu maswali hayo.

(b) Watahiniwa wasisitizwe kufanya maandalizi ya kutosha kupitia njia mbalimbali kama kusoma vyanzo mbalimbali vinavyohusiana na mada za Maarifa ya Jamii.

(c) Wakati wa ufundishaji na ujifunzaji, wakufunzi waweke mkazo katika mada zote za Taaluma na Ufundishaji kwenye masomo ya Historia na Jiografia ili kuleta uwiano mzuri wa ufaulu katika mada husika.

(d) Wakufunzi waweke mkazo katika matumizi ya mbinu shirikishi hususani, mbinu ya majadiliano na kazi mradi katika mada ya Utawala na Uchumi wa Kikoloni Afrika ambayo imeonekana kuwa na kiwango cha chini cha ufaulu ikilinganishwa na mada nyingine ili kuwajengea wanachuo uwezo mkubwa wa kuwasilisha hoja zao kwa kuongea na kimaandishi na hivyo kuwasaidia kujibu vizuri maswali ya insha katika mtiririko unaotakiwa wawapo vyuoni na hatimaye katika mtihani wa Taifa.

## MUHTASARI WA UFAULU WA WATAHINIWA KATIKA SOMO LA MAARIFA YA JAMII

| Na. | Mada | Na. ya swali | Ufaulu Katika Kila Swali (%) | Wastani wa Ufaulu Katika Kila Mada (%) | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Maandalizi ya ufundishaji na ujifunzaji | 16 | 97.7 | 97.7 | Vizuri |
| 2. | Ufundishaji na ujifunzaji wa somo | 15 | 98.4 | 97.4 | Vizuri |
| 3. | Mabadiliko Ya Kijamii, Kisiasa Na Kiuchumi KatikaAfrika Huru | 6 | 96.8 | 96.8 | Vizuri |
| 4. | Asili na mabadiliko Ya Binadamu, Teknolojia na Mazingira. | 13 | 95.8 | 95.8 | Vizuri |
| 5. | Sayari Dunia | 5 | 96.2 | 94.6 | Vizuri |
| | | 3 | 93 | | |
| 6. | Ushirikiano wa Kimataifa | 9 | 93.1 | 93.1 | Vizuri |
| 7. | Stadi Sahili na Tata za Picha na Ramani | 1 | 66.6 | 83.1 | Vizuri |
| | | 12 | 99.7 | | |
| 8. | Nchi Yetu Tanzania | 2 | 48.7 | 82.1 | Vizuri |
| | | 4 | 98.6 | | |
| | | 11 | 99 | | |
| 9. | Vitangulizi vya Ukoloni Tanganyika, Zanzibar na Kwingineko Afrika | 10 | 79.1 | 79.1 | Vizuri |
| 10. | Ukombozi wa Bara la Afrika | 7 | 79.1 | 79.1 | Vizuri |
| 11. | Utawala na Uchumi wa Kikoloni Afrika | 8 | 58.9 | 51.4 | Watani |
| | | 14 | 43.9 | | |